# SERIKALI YA MAPINDUZI ZANZIBAR
# MAHKAMA

## TANGAZO LA MAOMBI YA UWAKILI NA UVAKILI

Mahkama ya Zanzibar inawakaribisha wale wote wenye sifa za kuomba uwakili na uvakili kuwasilisha maombi yao kupitia mfumo ***advocates.judiciaryzanzibar.go.tz*** si zaidi ya tarehe 31/05/2025. Udahili kwa waombaji wenye sifa utafanyika Juni, 2025.

### SIFA ZA WAOMBAJI WA UWAKILI

***Kwa wazanzibari:***

1. Awe amehitimu shahada ya sheria katika chuo kikuu kinachotambuliwa na Serikali, na
2. Kwa aliyemaliza shahada ya sheria kuanzia 2018 na kuendelea, anatakiwa pia awe amehitimu stashahada ya uzamili ya sheria kwa vitendo kutoka Skuli ya Sheria ya Zanzibar au chuo chengine kinachotambuliwa na Baraza la Mawakili.

***Kwa wasio wazanzibari:***

Awe ni wakili kutoka Tanzania Bara, Kenya, Uganda, Rwanda, Burundi, na nchi nyengine za Jumuiya ya Madola, na amefanya kazi za uwakili kwa kipindi kisichopungua miaka mitano mfululizo.

### VIAMBATANISHO KATIKA MAOMBI YA UWAKILI

1. Nakala ya cheti cha shahada ya sheria,
2. Nakala ya matokeo ya kitaaluma (Transcript),
3. Nakala ya cheti cha stashahada ya uzamili ya sheria kwa vitendo,

4. Nakala ya vyeti vya elimu ya sekondari,
5. Nakala ya cheti cha kuzaliwa,
6. Kwa mzanzibari nakala ya kitambulisho cha mzanzibari,
7. Kwa ambaye sio mzanzibari nakala ya kitambulisho cha taifa au hati ya kusafiria (kwa waombaji kutoka Tanzania Bara, Kenya, Uganda, Rwanda, Burundi na nchi nyengine za Jumuiya ya Madola),
8. Nakala ya cheti cha usajili wa wakili,
9. Barua ya mdhamini,
10. Uthibitisho wa tabia nzuri ya muombaji.

**SIFA ZA WAOMBAJI WA UVAKILI**

1. Awe na stashahada ya sheria kutoka katika chuo kikuu au taasisi inayotambuliwa na Serikali, na
2. Awe amepata mafunzo maalum ya masuala ya sheria kwa kipindi kisichopungua miezi mitatu kutoka katika Skuli ya Sheria ya Zanzibar au yengine kama hiyo inayotambuliwa na Baraza la Mawakili.

**VIAMBATANISHO KATIKA MAOMBI YA UVAKILI**

1. Nakala ya cheti cha stashahada ya sheria,
2. Nakala ya matokeo ya kitaaluma (Transcript),
3. Nakala ya vyeti vya elimu ya sekondari,
4. Nakala ya cheti cha mafunzo maalum ya masuala ya sheria kwa mavakili,
5. Nakala ya cheti cha kuzaliwa,
6. Nakala ya kitambulisho cha mzanzibari,
7. Barua ya mdhamini,
8. Uthibitisho wa tabia nzuri ya muombaji.

MAHKAMA KUU No. 2 ZANZIBAR

.............................

**VALENTINA A. KATEMA**
**MRAJIS WA MAHKAMA KUU**
**ZANZIBAR**